



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA MANISPAA MPANDA**



Unapojibu Tafadhali taja:

**Kumb. Na. KTV/MMC/A.40/3**

**Tarehe: 22/02/2022**

**YAH: TANGAZO LA NAFASI YA KUKUSANYA TAARIFA ZA MFUMO WA  
ANWANI ZA MAKAZI NA POSTIKODI.**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda, anapenda kuwatangazia nafasi za ajira ya muda mfupi kwa nafasi za wakusanya taarifa kwenye zoezi la anwani za makazi katika kata, Vijiji na Mitaa yote ya Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda.

**A. SIFA ZA MWOMBAJI**

- i. Awe raia wa Tanzania mwenye umri kati ya miaka 18 hadi 40.
- ii. Awe na elimu kuanzia kidato cha nne na kuendelea.
- iii. Awe anamiliki simu janja (Smartphone) inayotumia mfumo wa Android na yenye uwezo wa kukaa na chaji kwa siku nzima.
- iv. Awe na barua pepe (Email Address) na Nywila (password) inayofanya kazi.
- v. Awe na Kitambulisho cha NIDA au namba ya NIDA
- vi. Awe na uwezo wa kusoma ramani za mitaa na Vijiji.
- vii. Awe ni mkazi wa kata husika.
- viii. Awe na uwezo wa kufanya kazi kwa muda mrefu.

**B. KAZI NA MAJUKUMU**

- i. Kukusanya taarifa za nyumba, viwanja na maeneo yote ya huduma.
- ii. Kukusanya taarifa za wamiliki wa nyumba, wategemezi, viwanja na maeneo ya huduma ya jamii kwa kutumia mfumo wa anwani za makazi.
- iii. Kutuma data kwenye mfumo wa anwani za makazi.
- iv. **Malipo yatafanyika kwa kuzingatia kiasi cha kazi kwa siku**

**C. MAOMBI YAAMBATANISHWE NA:**

- Nakala ya cheti cha kuzaliwa
- Nakala ya cheti cha kidato cha nne
- Picha 2 za passport size za hivi karibuni
- Barua ya maombi ipitishwe na Mtendaji wa Kata au Mtaa/Kijiji anapoishi

**D. JINSI YA KUTUMA MAOMBI**

Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na anwani kamili ya mwombaji, namba ya simu na barua pepe: Maombi yote yawasilishwe kwa njia ya mkono kwenye ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Mpanda kwa anwani ifuatayo:

Mkurugenzi wa Manispaa

Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda

S. L. P 216

**MPANDA**

**E. TAREHE YA MWISHO KUPOKEA MAOMBI.**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 25/02/2022 saa 9:30 Alasiri.

SOPHIA J. KUMBULI  
**MKURUGENZI WA MANISPAA  
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MPANDA**

MKURUGENZI WA MANISPAA  
MANISPAA YA MPANDA  
S.L.P 216  
MPANDA-KATAVI